



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI



Kumb. Na LMC/J.20/3/VOL.III/64

Tarehe 22/06/2023

TANGAZO LA NAFASI YA AJIRA YA MKATABA YA MWAKA MMOJA (1)

Shule ya Sekondari Lindi Wasichana ni miongoni mwa Shule Mpya 10 zilizojengwa na Serikali ya Awamu ya Sita katika Mikoa 10 ya Tanzania Bara. Shule ni ya Bweni Maalum ya Sayansi kwa wanafunzi wa Kike. Shule hii ina mandhari na mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia. Shule ya Sekondari Lindi Wasichana iko umbali wa mita 800 kutoka barabara kuu ya Lindi - Dar es saam, Mtaa wa Kilangala B, Manispaa ya Lindi na ipo umbali wa kilometra 40 kutoka Lindi Mjini. Shule hii inatarajia kuanza kupokea Wanafunzi wa Kidato cha Tano kunzia tarehe 13 Agosti, 2023.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi anapenda kuwatangazia Wananchi wote wenye sifa kuomba nafasi za Ajira ya Mkataba wa mwaka mmoja (1) kwa nafasi zifuatazo: -

1. MLINZI DARAJA LA II NAFASI 3

Sifa za Mwombaji.

Kuajiriwa Wahitimu wa Kidato cha Nne, waliohitimu Mafunzo ya Mgambu/Polisi/JKT au Mafunzo ya Zimamoto kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

Majukumu ya kazi ya Mlinzi Daraja la II.

- i. Kuhakikisha kwamba mali yoyote ya Ofisi inayotolewa langoni (Nje ya Ofisi) ina hati ya idhini.

Ofisi ya Mkurugenzi, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, S.L.P 1070 Lindi, Simu: +255 023-220-2164, Nukushi: +255 023-220-2116, Barua pepe: info@lindimc.go.tz, Tovuti: www.lindimc.go.tz

- ii. Kuhakikisha kuwa, mali yote inayoingizwa langoni inazohati za uhalali wake.
- iii. Kulinda usalama wa Majengo, Ofisi na Mali za Ofisi mchana na usiku.
- iv. Kuhakikisha kwamba milango na madirisha yote yamefungwa ipasavyomwisho was aa za kazi.
- v. Kuhakikisha kwamba wageni wote wanaingia katika eneo la Ofisi wana idhini ya kufanya hivyo.
- vi. Kupambana na majanga yoyote yatakayotokea katika eneo la kazi kama vile, moto, mafuriko na mengine na kutoa taarifa katika vyombo vinavyousika, kama vile Polisi na Zimamoto.
- vii. Kutoa ushauri jinsi ya kuboresha huduma ya ulinzi mahali pa kazi.

Ngazi ya Mshahara:

Mshahara utalipwa kwa viwango vya Serikali ambavyo ni TGOS A.

2. MPISHI DARAJA LA II NAFASI 2

Kuajiriwa Wahitimu wa Kidato cha Nne, waliohitimu Mafunzo ya Upishi kutoka katika Chuo cha VETA au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

Majukumu ya kazi ya Mpishi Daraja la II.

- i. Kuandaa na kuwapikia wanafunzi chakula kwa kufuata ratiba ya chakula aliyopewa.
- ii. Kufanya usafi wa vyombo, jiko, na maeneo yake kama stoo na eneo la kuoshea vyombo.
- iii. Kuhakikisha kuwa vyakula vilivyoletwa na wanafunzi/wazazi ni salama na vinahifadhiwa katika hali ya usafi.
- iv. Kuhakikisha usalama na usafi kwa vyakula vyote vilivyopikwa.
- v. Kuandaa vitafunwa mbalimbali na wanafunzi kama inavyooneshwa kwenye ratiba.
- vi. Kuwasimamia wanafunzi kusafisha na kuhifadhi vizuri vyombo vyao vya kulia na kuhifadhi chakula.

Ngazi ya Mshahara:

Mshahara utalipwa kwa viwango vya Serikali ambavyo ni TGOS A.

3. MHUDUMU WA JIKONI DARAJA LA II NAFASI 2

Sifa za Waombaji.

Kuajiriwa wahitimu wa Kidato cha Nne wenyewe uzoefu wa kazi kwa muda usiopungua miaka mitatu.

Majukumu ya kazi ya Mhudumu wa Jikoni Daraja la II.

- i. Kuandaa na kuwapikia wanafunzi chakula kwa kufuata ratiba ya chakula aliyopewa.
- ii. Kusafisha vyombo vya kupikia
- iii. Kusafisha vyombo vya kulia chakula
- iv. Kusafisha Meza zitumiwazo kwa chakula
- v. Kuwatayarishia Wapishi/Waandazi vifaa vya Mpishi na Mezani.
- vi. Kusafisha maeneo ya kulia chakula na kupikia.
- vii. Kuwasaidia Waandaaji na Wapishi.

Ngazi ya Mshahara:

Mshahara utalipwa kwa viwango vya Serikali ambavyo ni TGOS A.

MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania.
- ii. Waombaji wote wawe na umri kati ya miaka 18-45.
- iii. Waombaji wote waambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- iv. Waombaji waambatishe Maelezo binafsi (CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika na majina mawili (2) ya Wadhamini.
- v. Maombi yote yaambatishwe na picha moja (Passport size ya hivi karibuni na iandikwe jina kwa nyuma).

- vi. Maombi yaambatishwe na nakala za vyeti vya Taaluma/Shule na vyeti vya kuhitimu mafunzo ya vyuo.
- vii. Waombaji wote waambatishe nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) kwa ambao hawana Vitambulisho hivyo, namba za NIDA ziandikwe kwenye maelezo binafsi (CV).
- viii. Maombi yote yatakayoambatishwa na Taarifa ya Matokeo ya Kidato cha Nne (Results Slip) hayatafanyiwa kazi.

UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI

Maombi yote yatumwe kwa Anuani ifuatayo:

Mkurugenzi wa Manispaa,
Halmashauri ya Manispaa ya Lindi,
S.L.P 1070,
LINDI.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 02/07/2023 Saa 9.30 Alasiri.

Juma A Mnwele
**MKURUGENZI WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA
LINDI.**

